KANUNI ZA MAADILI NA MAKUBALIANO KWA KILA MSHIRIKI WA RALEIGH INTERNATIONAL

Jina:..... **No. Ya Utambulisho.....**

(kwa matumizi ya ofisi tu)

1. UTANGULIZI

Tunataka washiriki wote wakubali na kuishi kulingana na makubaliano na tutatoa mafunzo na uwezeshaji kuhakikisha inafanikiwa. Lengo kubwa la makubaliano haya ni kujua nini kinategemewa kutoka kwenu ili kufanya kazi kwa pamoja na kwa ukaribu kati yenu na malengo ya mradi ili kuleta malengo chanya na mazingira salama.

Unatakiwa kusoma sheria na makubaliano ya Raleigh International wakati unapojiunga na mradi huu, hivyo utasaini nakala ya makubaliano haya kabla ya kuondoka au wakati wa mafunzo kabla ya kwenda maeneo yenu kwa ajili ya kuanza mradi. Nakala hii itasiniwa na wewe mwenyewe kwa usimamizi wa mtu mwingine kutoka Raleigh na itahifadhiwa katika kipindi chote utakapo kuwa Raleigh. Haya makubaliano sio ya kisheria wala sio mkataba wa kisheria.

Kujitoa katika pia hakuta kugharimu kifedha tu bali kutaleta mkanganyiko kwa timu yako nzima na pia jamii uliyopangiwa kwenda kuisaidia. Utatumia muda wako mwingi na hata nguvu zako nyingi katika maandalizi ya mradi ***kwahiyo ni muhimu kusoma na makubaliano haya kwa umakini na uangalifu mkubwa kabla ya kusaini na kujiridhisha na mradi..***

Mradi utakuwa ni nafasi nzuri kwako kuwa balozi mzuri wa nchi yako na hata pia kwa Raleigh. Tunaanglia mbele kufanyakazi nawe na tunatarajia utafanya na kutumia nafasi hii vizuri.

2. VIPIMO KWA WASHIRIKI

Hatuangalii vigezo maalumu wala elimu kwa washiriki wetu, hivyo tunachoangalia ni watu ambao wako tayari kujifunza mambo mbalimbali ili kuja kuwa wananchi walio hai katika jamii na nchi kwa ujumla. Kuna maeneo 7 ambayo tunaangalia ambayo ni:

a) **Kukubali na kuwatayari**
   Unatakiwa kuwa tayari mwenye mtazamo chanya kufanya kazi kwa kujitolea ili kuleta mafanikio yatakayoonekana.
b) **Kuwa tayari kujifunza**
   Unatakiwa kuwa na malengoe ndelevu ya kujifunza mambo mapya na pia kuendeleza wengine.
c) **Kuwa na uwezo wa kutatua matatizo kwa vitendo**.

Uwezo wakutatua matatizo mbalimbali kwa kutumia nyenzo zilizopo, na kufanya mambo chanya katika kufanya maamuzi panapostahili.

d) Mabadiliko na utambuzi

Kukubali mabadiliko kulingana na mahitaji ya sehemu au mazingira mbalimbali.

e) Kujiamini

Kujiamini katika kufanyakazi na watu a aina tofauti ukiwa huru mwelevu ,kwa upole na busara pia.

f) Kufanyakazi na wengine

Uweze kufanya kazi na watu wengine hasa jamii na kuwasidia katika kutatua matatizo mbalimbali ili kuhakikisha malengo yao yanafikiwa.

g) Ufahamu juu ya mahitaji ya wengine.

Uwezo wakuheshimu watu wengine na hata tamaduni zao. Uwezo mzuri wa kusikiliza na utulivu.

Katika kipindi chote utakachokuwa Raleigh ni muhimu kuonesha uhitaji wako na utayari wako katika kuendeleza hizi sheria na haya mazingatio. Kinyume na hapo utakuwa umeshindwa au umevunja makubaliano na sheria za Raleigh kama ilivyo katika kifungu cha 5

3. UNATEGEMEA NINI KUTOKA RALEIGH

kwakuwa program hii inahitaji kiasi kikubwa cha utayari kutoka kwako na piakiasikikubwa cha fedhakutokakwetunivyemakusemanikituganiunategemeakutokakwetu.

3.1.Kablaya program unategemeakuapatavifuatavyo

- Maelezo yanayoelezea mradi na yanayohusika na hatari inayoweza kuwepo katika eneo lako la kufanyia kazi.
- Mwendelezo wa maelezo,, uwezeshaji, ana ushauri kutoka kwa timu nzima ya uwezeshaji wa wanaojitolea (volunteers) kutoka ofisi kuu.

3.2 Katika programu

- Kutoa malazi, chakula, usafiri na uwezeshaji kuwezesha utekelezwaji wa mradi. Tutaangalia mabadiliko ya hatari zinazoweza kuathiri maendeleo ya mradi, hata hivyo tutaangalia mipaka ya Raleigh kuweza kuzuia hizo hatari katika kila mradi.
- Kuwahakikishia kila kilichoahidiwa kabla ya kuondoka kwenda katika maeneo yenu.
- Uwezeshaji wa kujifunza hasa katika rasilimali na mafunzo
- Kuahakikisha usawa kwa wote.

3.2.Mara baada ya programu

- Kupata taarifa ya baada ya kumaliza
- Washiriki wa ICS watapewa siku ya mapito (review day) kuhusu programu
- Kukuongeza katika kundi la mtandao (Almin network) ambao una watu zaidi ya 43,000 na kukutumia taarifa zaidi kuhusu programu.

4. RALEIGH INATEGEMEA NINI KUTOKA KWAKO?

4.1.Kabla ya programu unatakiwa:

- Kusoma na kuelewa taarifa zote ambazo Raleigh watakuwa wakitoa kwako na kufanya mambo yaote unayoelekezwa kufanya kwa usahihi kama vile utakavyoelekezwa kufanya na kwa muda husika.
- Kufanya maamuzi yaliyothibitishwa, kulingana na taarifa iliyotolewa na Raleigh na kukusanywa ili kuhepusha matatizo na hatari mbalimbali katika programu. Hata hivyo hizi hatari zinaweza kuangaliwa hasa katika maeneo ya kuishi na kufanyiia kazi hivyo basi hizi hatari ni za watu walio katika programu.
- Kufanya kilia uwezalo kuhakikisha unachangia Raleigh kwa naman moja au nyingine. Hizi pesa hazitarudishwa endapo utaamua kuondiika au kuikacha programu kwa hiari yako mwenyewe.
- Unatakiwa kujiamini katika masuala yote ya upishi, afya kwa ujumla, usafi na umakini kwa ujamla.

4.2. kama balozi wa Raleigh na nchi yako tunategemea ndani ya kipindi chote cha programu utaendeleza na kuishi tabia za kimataifa za Raleigh. Kama utashindwa kufanya hivyo, Raleigh itachukua hatua. Angalia kifungu cha 5.

TABIA ZA KIMATAIFA ZA RALEIGH

Hakuna kunywa pombe. Mazingira ya ndani ya nchi yanaweza kuwa ni hatari sana. Timu za Raleigh pia ni mabalozi wa nchi zao wenyewe na pia hata nchi wenyeji wao, hivyo ni muhimu kwa washiriki wote kuwa na tabia nzuri, kufanya maamuzi na hukumu vizuri na kutengeneza mazingira yatayohakikisha usalama wao na wengine**.** Hivyo basi utumiaji wa pombe wakati wa mradi hauruhusiwi kabisa kwa watu wote bila kujali umri wala cheo.

Hakuna shughuli zisizo za kisheria, ikiwemo matumizi ya madawa ya kulevya au utumaiaji wa dawa bila ya maelekezo ya mtabibu toka Raleigh. Kwa nchi nyingi ambazo tunafanya kazi matumizi ya madawa ya kulevya, kuuza madwa ya kulevya, kununua, hata bangi ni kosa na pia huwa adhabu kubwa zinatolewa na hata muda mwingine huwa na adhabu ya kifo. Kushiriki katika kazi yoyote isiyo ya kisheria ambayo inaweza ikahusisha hata jamii husika kwa namna yoyte ile inaweza kukusababishia kutolewa nje ya progam nzima inayokuhusu. Kuvunja sheria yoyote ya nchi iinaweza kukusababisha kukutana na vyombo vya sheria.Vivo hivyo pia hairuhusiwi kuchukua wala kutumia dawa kutoka kwenye sanduku la dawa la Raleigh bila ya ruhusa kutoka kwa mtabibu wa ofisi.

Hakuna vitendo vya unyanyasaji. Kufanya kazi kama timu ni kitu kizuri zaidi na ndio kinategemewa zaidi pindi muwapo katika program hivyo vitendo vya unyanyasaji vya aina yoyote baina ya washiri wa timu au hata na jamii husika haviruhusiwi na havitavumiliwa. Vitendo hivyo vinaweza kuwa kwa maneno, vitisho, au hata maneno ya kashfa havitaruhusiwa.

Usiwaweke wenzako katika hatari . Angalia tabia yoyote ile iliyonayo isiwaweke wenzako katika hatari ya aina yoyote ile, au hata kuwanyima raha wengine au hata kusitisha maendeleo ya mradi. Raleigh ina mwongozo na ungalifu mkubwa sana katika masuala ya ulinzi na usalama ambazo zinatoa taarifa kwa kila kazi tunayofanywa kwa kutumia uzoefu wetu tulionao kwa miaka 30 tuliyokuwa tukifanya programu zetu na kutufanya kuwa shirika linaloongoza katika masuala mazima ya usalama kwa watu wanaojitolea kutoka Uingereza kuja nchi na kuishi katika maeneo ya vijijini.kila mtu atayekuwa Raleigh anatakiwa kukubaliana na makubaliano haya. Kibaya zaidi kuumwa au majeraha yanayoweza kusababishwa na kutokuzingatia kwa makubaliano ya ulinzi na usalama wa washiriki yanaweza kusababishwa kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mahusiano ya kimapenzi kati ya kiongozi wa timu (Team Leader/Project Manager) na washiriki(Volunteers) hayaruhusiwi kabisa. Kutakuwa na melezo na pia hata mwongozo mzima kutoka kwa viongozi wa timu wakati wa mradi hivyo basi mahusiano ya aina yoyote ya kimapenzi kati ya viongozi wa timu (team leaders/ volunteer managers/Deputy Operations Managers / Country Office Volunteers) na Volunteers hayaruhusiwi kabisa katika kipindi kizima cha mradi vilevile washiriki mbali mbali wa Raleigh kama (Volunteer Managers / Team Leaders / Duty Operations Managers / Country Office Volunteers na Volunteers) na wana jamii, washiriki wa mradi na watoa huduma. Hii haijalishi umri wa washiriki.

Kuheshimu mila na desturi za jamii husika. Kwa wale wageni wote wanaotoka nje ya nchi wanatakiwa kukubali mazingira wanayoyakuta na kuheshimu wale wote waliokubali kuishi katika nchi yao. Tunayo meni ya kuifunza kutoka tamadudi na tabia mbalimbali za watu na ukiwa kama balozi wan chi yako na ukiwa kama mgeni katika chi yao ni muhimu kelewa na kuheshimu tamaduni za jamii zao na kuziheshimu kwa muda wote.

Chukua picha tu acha nyayo. Huu msemo una maana ya kwamba Matokeo mazuri zaidi ya mradi huwa kwa mazingira husika na pia kwa jamii husika pia hivyo basi unatakiwa kupunguza uharibifu wowote wa mazingira ambao unaweza kwa hiyo ni muhimu kuheshimu na kutunza mazingira kwa ajili ya matumizi ya baadae kwa wengine.

Kuwalinda watoto. Kuna baadhi ya washiriki wa programu za Raleigh wako na umri mdogo yaani chini ya umri wa miaka 18 hivyo katika jamii husika tunazofanya nazo kazi huwa wanachukuliwa kama watoto. Kwa hiyo tuko makini zaidi kulinda sera za watoto na hivyo amechaguliwa mtu maaluum kwa ajili ya kuhakikisha na kulinda haki za watoto ili wasije wakapatwa ma matatizo ya aina yoyote kama kuumia au hata kupata majeraha ya aina yoyote pindi watakapokuwa katika maeneo yao ya kazi huko katika jamii husika. Washiriki wote wa program za Raleigh wanatakiwa kuheshimu sera hii.

Nafasi / Fursa sawa. Raleigh inajitahidi kufanya shughuli zake katika fursa ya usawa na pia imejidhaatiti na kujikamilisha kuchukua hatua zozote zile za msingi na mifumo ili kuhakikisha kuna fursa sawa kwa vijana wote bila ya kujali jinsia, umri, kiwango cha maendeleo, ulemavu, mahusiano, dini, tamaduni, mila, hata kabila.

Ustawi. Washiriki wote watakaokuwa katika progam zinazoendeshwa Raleigh au hata wale ambao watavutiwa na kazi zetu wanatakiwa kuwa wazi bila ya kuogopa kitu chochote au kitisho cha aina yoyote. Viongoi wote na washiriki wote wanatakiwa kuheshimu na na kuelewa haki za vijana na usawa au haki na wanatakiwa kuwa pivha au mfano kwa sheria zote za Raleigh kwa muda wote. Raleigh inafanya kazi ili hata kuhakikisha usawa wa watu wote, kupinga ubaguzi ndio maana inafanya kazi na watu wa kutoka tamaduni na sehemu mbalimbali ili kuonesha usawa huo katika ufanyaji wa kazi kwa pamoja.

Picha. Raleigh huwa inatunmia aina yoyote ya picha au video ambazo unaweza kuzituma au kuzitoa kwa mtu yoyote aliye ofisini wakati wa programu au hata baada ya programu ikiwa ni matokeo ya programu kwa kupitia mtandao wetu. Ni wajibu wako kuhakikisha unaruhusa ya kumshirikisha mtu yoyote kwa picha na video unazotutumia.

Teknolojia ya mawasiliano. Raleigh ina sera ya kutowaruhusu watu wake au washiriki wake kutotumia simu za mkononi au laptops pindi wanapokuwa maeneo ya vijijini au sehemu za miradi isipokuwa tu imeruhusiwa na miradi ya ICS. Vijiji tunavyofanyia kazi viko ndani sana na na pia vyenye watu wa kila aina na uchumi wake ni wa chini sana ingawa sio kila wakati ni uhakikisho wa maisha waliyonayo. Tunaamini kwamba kuwa mbali na watu (kimawasiliano) inakupa muda mzuri wa wa kielewa na kuisoma jamii na mazingira uliyopo. Kwa kuongezea uwezo wako wa kutunza na na nzuri zaidi na ukizingatia ya kwamba bima inayotolewa na Raleigh haizingatii upotevu wa vitu binafsi. Lakin pia hii haimaanishi ya kwamba hakutakuwa na mawasilino na nyumbani kwanu bali wafanyakazi wa Raleigh wataskushauri namna ya kufanya mawasiliano ya haraka endapo kuna dharura ya aina yoyote imetokea katika maeneo yenu ya kufanyia kazi.

Hizi ni baadhi ya kanuni za maadili;

- Kutoshiriki katika shughuli yoyote ambayo inaenda kinyume na malengo ya mradi..
- Kutokujihusiha na Shughuli yoyote ambayo haitakua na manufaa kwa mradi.
- Kutoshiriki katika shughuli yoyote yenye manufaa binafsi
- Kuomba lifti kwa watu usio wafahamu
- Kutoendesha chombo chochote cha moto isipokuwa kwa ruhusa kutoka ofisi za Raleigh.
- Kutopanda pikipiki ya aina yoyote au kuendesha gari na kutokutumia baiskeli kama muendeshaji au kubebwa.
- Huruhusiwi kujitia tatoo mwilimi au kujitoboa kwa namna yoyote uwapo ndani ya mradi.
- Shiriki kwa ukamilifu katika mradi na pia unatakiwa kuzingatia kuwa mambo yanaweza kubadilika kulingana na mazingira na sehemu utakayopangiwa na hakuna uzoefu wala vigezo maakum vya kuzingatia katika hilo.

- Kutotumia compyuta au kuchukua taarifa za aina yoyote kwa kutumia flash bila ya ruhusa ya mmliki husika au kwa namna isiyofaa.
- Kutomiliki au kusambaza picha za ngono
- Kutorudi nyumbani katikati ya mradi, isipokuwa tu endapo kuna dharura za kifamilia na ikiwa tu kwa idhini ya viongozi wa Raleigh.
- Kurudi nyumbani (UK) kwa usafiri uliopangwa na na shirika la kimataifa la Raleigh (kwa UK volunteers tu)
-

UKISHINDWA KUFUATA KANUNI ZA MAADILI ZA RALEIGH

Endapo kanuni hizi hazitafuatwa kuna utaratibu wa kutoa onyo hufanyika mabo uko katika namna tatu ;

- Onyo kwa mdomo
- Onyo kwa maandishi
- Kuondolewa kwenye mradi.

Adhabu ya kuondolewa kwenye mradi iitatolewa pale tu uvunjaji wa lazima utakapotokea. Ingawa maamuzi ya mwisho ya jinsi ya tutakavyopokea uvunjifu wa sheria na taratibu zilizotajwa hapo juu, ni juu ya wafanyakazi na viongozi kutoka makao makuuyaliyapo London. Kama unatakiwa kuondoka katikati ya mradi utahusika na zote za usafiri.

6. HITIMISHO

Mafanikio ya programu yanategemea na jinsi washiriki wanavyochukuliana kila mmoja na wenyeji wa jamii husika na kwa heshima ya hali ya juu. Madhara ya tabia zisizofaa kwenye mabadilishano ya kitamaduni si rahisi kwa washiriki kuona kwa maramoja au hata kuelewa kwa kipindi cha muda mfupi. Maamuzi ambayo yanayoonekana ni ya busara kwa mtu mmoja au kikundi kidogo cha watu pia wakati mwingine yanaweza kuathiri programu nzima. Ili kusaidia kulinda dhidi ya matatizo haya washiriki wote lazima wakubaliane na hizi kanuni za maadili, Katika uwezo wetu haya ndio yanajenda misingi imara ya mafanikio ya programu.

7. MAKUBALIANO

Nimesoma na kukubaliana kikamilifu na maelezo yaliyotajwa hapo juu, na taarifa zote zilizo tolewa na shirika la kimataifa la RALEIGH.

Kwa kusaini mkataba huu, nathibitisha kukubaliana na programu ya SHIRIKA LA RALEIGH.

Saini ya Mshiriki

Jina.....

Saini.....

Tarehe.....

Saini kwa niaba ya RALEIGH

Jina.....

Saini.....

Tarehe.....